**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

# SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

02/10/2025

## TAARIFA KWA UMMA

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inapenda kuwakumbusha viongozi wote wa umma walioainishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Sura ya 398), kuwa upokeaji wa Tamko la Rasilimali Maslahi na Madeni kwa mwaka 2025, umeanza tarehe 01 Oktoba, 2025 na utamalizika tarehe 31 Desemba, 2025.

Uwasilishaji wa Tamko hilo kwa Kamishna wa Maadili ni kwa mujibu wa kifungu cha 9 (1) (b) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kwamba kutoa Tamko la uongo, kuchelewa ama kushindwa kuwasilisha Tamko hilo kwa kipindi kilichoainishwa kisheria ni ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria tajwa.

Aidha utoaji wa tamko hilo unafanyika kwa njia ya mtandao (***Online Declaration system – ODS***).

Viongozi ambao walishawahi kutoa Tamko kwa njia ya mtandao watatumia taarifa *"credentials"* walizotumia awali na kuendelea na utoaji wa Tamko. Kiongozi ambaye hajawahi kutoa Tamko atatakiwa kuingia kwenye mfumo kupitia anuani ***ods.maadili.go.tz*** na kubofya kitufe kilichoandikwa ***jisajili*** kisha atafuata maelekezo yatakayomsaidia kujisajili na kuendelea na zoezi la utoaji wa Tamko husika.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa kupitia barua pepe ***helpdesk@maadili.go.tz. au simu +255262160190 / +255262160192 / +255734101040.***

Imetolewa na:

Jaji (Stahiki) Sivangilwa S. Mwangesi
**KAMISHNA WA MAADILI**

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
**Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura**

Jengo la Maadili, 1 Mtaa wa Maadili, S.L.P 225, Dodoma, Simu: 026-2160190, Barua pepe: ec@maadili.go.tz
Tovuti: https://www.maadili.go.tz